

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MJINI GEITA**



MKATABA NA. GEUWASA/AE/082/2021/2022/W/04

KWA AJILI YA

UJENZI WA TENKI KWA AJILI YA KUPANUA MTANDAO WA
MAJI KWENYE MJI WA GEITA (ENEO LA IGEMBESABHO)

KATI YA

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MJINI GEITA**

"MWAJILI"

NA

BW. RICHARD JAMES MALIMA

"MWAJILIWA/FUNDI"

NOVEMBA, 2021

SEHEMU YA I: FOMU YA MAKUBALIANO YA MKATABA

Makubaliano haya ya Mkataba yanafanywa leo tarehe 08 mwezi wa 11, 2021. Kati ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita S.L.P 477 GEITA (Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja na Ally Joseph Method S.L.P 40562 Geita (Hapa ataitwa "Mkandarasi") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Mwajiri anataka baadhi ya kazi zifanyike yaani: UJENZI WA TENKI KWA AJILI UYA KUPANUA MTANDAO WA MAJI KWENYE MJI WA GEITA (ENEO LA IGEMBESABHO) na kwa barua ya kukubali yenye Kumb Na. GEUWASA/COVID19/VOL.01/08ya tarehe 01/11/2021 alikubali zabuni ya Mkandarasi kwa utekelezaji na ukamilishaji wa kazi hiyo.


SASA MAKUBALIANO HAYA YAMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:

1. Katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaorejelewa na;
2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani;
 1. Fomu ya Makubaliano ya Mkataba;
 2. Barua ya Kukubali Kotesheni;
 3. Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni;
 4. Masharti Maalumu ya Mkataba;
 5. Masharti ya Jumla ya Mkataba;
 6. Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi;
 7. Michoro;
 8. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa).
3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo baadae kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.
4. Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa Mkandarasi kama baadaye inavyotajwa, Mkandarasi hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha kazi kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote kulingana na vifungu vya mkataba.


Mwajiri hapa anakubali kumlipa Mkandarasi kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi, jumla ya fedha za Tanzania Shilingi Milioni Ishirini Mia Tano Thelathini na Nne Elfu Mia Tano (TZS 20,534,500) baadaye imerejelewa kama 'Bei ya Mkataba' kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

KATIKA KUSHUHUDIA, pande hizi zimekubaliana na kutia sahihi na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**IMETIWA SAHIHI KWA AJILI YA
NA KWA NIABA YA MWAJIRI**



Sahihi
(Jina) **FRANK GHANGAWA**
(Kazi) **MANAGING DIRECTOR**



Mbele ya



Sahihi
(Jina) **Ashrafu Bantule**

(Kazi) **Mwajiri Kwa Niaba**

KWA NIABA YA MKANDARASI:




Sahihi
(Jina) **RICHARD JAMES MALIMA**

(Kazi) **FUNDI**

(Anwani) **0964087522**



Mbele ya



Sahihi
(Jina) **ALLY JOSEPH METHO**

(Kazi) **FUNDI**

(Anwani) 